



Code 0012020

# THE TIMER NATIONAL SERIES

## MONITORING LEARNERS' PROGRESS

Grade 4 - 2020

### KISWAHILI ACTIVITIES

JIN.....

Learner's Number

Gender Boy

Girl

County name ..... County code

Sub county name ..... Sub county code

School name ..... School code




Mwalimu ajaze jedwali hili baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi

	Kiwango cha 1	Kiwango cha 2	Kiwango cha 3	Kiwango cha 4
Sehemu ya 1				
2				
3				
4				

## SEHEMU YA 1

### Kusikiliza na kuzungumza

Sema umuhimu wa vifaa hivi.



Taja miezi mitatu ya mwaka.

Eleza umuhimu wa mazingira.

## SEHEMU YA 2

### Kusoma

Halima ni mwanafunzi mzuri. Nyumbani kwao wana duka kubwa sana. Humo dukani wao huuza sukari, mikate, unga na mafuta. Jana kaka alinunua kilo tano za sukari na mikate mitatu. Alimpea muuzaji pesa kisha akaenda.

Alipofika nyumbani, mama alimuuliza, "mbona hukununua mafuta?" Kaka alisema mafuta yaliuzwa kwa bei ghali sana. Halima alitwambia kuwa duka lao huwapatia faida nyingi sana.

### Kusoma ufahamu

Twiga hupatikana katika maeneo ya kusini mwa africa, pamoja na Afrika mashariki- Kenya, Uganda na Tanzania. Ndiye mnyama mrefu zaidi duniani. Urefu wake ni kati ya mita nne nukta tatu na mita tano nukta nane. Uzito wa twiga ni kilo mia nane na elfu moja, mia mbili na hamsini. Aliye na uzito wa juu ni wa kiume.

Twiga ana maisha ya takribani miaka ishirini na mitano. Chakula chake ni nyasi na majani ambayo huyafikia kwa shingo lake ndefu sana. Ulimi wa twiga unafikia urefu wa centimita arobaini na tano.

Mtoto wa twiga azaliwapo ni mrefu kuliko mwanadamu aliyekomaa. Mtoto huyo anaweza kusimama baada ya dakika kumi. Baada ya saa kumi anaweza kukimbia kando ya wazazi wake.

Twiga ndiye alalaye kwa muda mfupi zaidi, kati ya dakika kumi na saa mbili kwa usiku. Twiga ana uwezo wa kulala huku akisimama na pia kuzaa akisimama. Yeye ni kivutio kwa watalii.

1. Taarifa hii inahusu mnyama gani? \_\_\_\_\_.
2. Taja eneo moja ambayo twiga hupatikana. \_\_\_\_\_.
3. Kati ya twiga wa kiume na wa kike, nani ana uzito wa juu? \_\_\_\_\_.
4. Ulimi wa twiga unafikia urefu wa centimita ngapi? \_\_\_\_\_.

Andika kweli au la


5. Twiga ana uwezo wa kulala huku akiwa amesimama. \_\_\_\_\_.

SEHEMU YA 3

Sarufi

Jaza 'juu ya' au 'chini ya'


1. Paka ako \_\_\_\_\_ meza.



2. Mpira uko \_\_\_\_\_ kiti.



3. Mtoto amelala \_\_\_\_\_ kitanda.



Jaza 'Huyu' au 'Hawa'

4. \_\_\_\_\_ ni wanaume.
5. \_\_\_\_\_ walimu wananipenda.

**SEHEMU YA 4**

**KUANDIKA**

**Andika insha juu ya:**

**MNYAMA NIMPENDAYE**

Lined writing area for the student's response.